# Prof. Ole Gabriel awafunda wasomi Hombolo

**Na Mbaraka Kambona, Dodoma**

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel amewaeleza wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa- Hombolo mkoani Dodoma kuwa wao ni viongozi watarajiwa hivyo wanawajibu wa kuhakikisha watakapokuwa viongozi wanakidhi matarajio ya wale watakaokuja kuwaongoza.

Prof. Gabriel aliyasema hayo wakati akiwasilisha mada iliyohusu nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii anayoiongoza kwenye hafla ya kuwatunuku zawadi wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao na watanyakazi bora wa chuo cha Hombolo iliyofanyika katika chuo hicho kilichopo Dodoma Novemba 25, 2020.

Alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho nchi ya Tanzania imeingia katika uchumi wa kati viongozi wanawajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wanakidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel aliongeza kuwa nchi nyingi na taasisi zimekuwa zikikwama kufikia malengo tarajiwa kwa sababu ya kukosa usimamizi mzuri.

"Kuwa na rasilimali ni jambo moja, lakini kusimamia rasilimali hizo ni jambo la muhimu zaidi, taasisi nyingi zimekwama kwa kushindwa kusimamia rasilimali zake ikiwemo rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali miundombinu," alisema Prof. Gabriel.

Kwa mantiki hiyo aliupongeza Uongozi wa Chuo cha Hombolo kwa kusimamia agenda ya uongozi huku akisema kuwa elimu hiyo wanayotoa kwa wanafunzi wa chuo hicho itawasaidia wanafunzi hapo mbeleni watakapokuwa viongozi.

Aliendelea kusema kuwa kiongozi yeyote wa kuchaguliwa au kuteuliwa ili awe kiongozi bora ni muhimu kuzingatia mambo matatu ambayo ni kufahamu hasa anaowaongoza wanamahitaji gani? pia Kiongozi atambue kuwa hatakumbukwa kwa cheo chake bali kwa mchango wake kwa jamii ile anayoiongoza na tatu, awe mtu anayeweshirikisha wale anaowaongoza katika kutatua changamoto zao.

"Washirikishe wale unaowaongoza na ndipo utakapoweza kutatua changamoto, kiongozi mzuri ni yule anayeiona changamoto na kuzibadilisha kuwa fursa, na kwa kufanya hivyo ndipo utaweza kukidhi matarajio ya wale unaowaongoza," alisisitiza Prof. Gabriel.

Katika hafla hiyo ya 12 ya chuo hicho, Prof. Elisante Ole Gabriel alikuwa Mtoa mada maalum na aliwasilisha mada hiyo ya nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa na wakuteuliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii ili kuwakumbusha wajibu wao mkubwa kwa jamii.



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (kulia) akifurahia jambo alipokuwa akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Elimu, Gereld Mweli (kushoto) walipokutana kwenye hafla ya kutunukiwa zawadi wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa- Hombolo waliofanya vizuri katika masomo yao. Prof. Elisante Ole Gabriel alikuwa mtoa mada maalum katika hafla hiyo iliyofanyika katika chuo hicho kilichopo Dodoma.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

ns
tis

for
ons

son
the
in
ad
m.
al
p-
ge
us
i-
i-

The National Newspaper

# DAILY NEWS

ISSN 0856-3812 No. 12,713 PRICE TShs 1,000/- KShs. 100 UShs 1,600 TANZANIA FRIDAY, NOVEMBER 27, 2020

@dailynewstz @dailynewstz www.dailynews.c

SPORT »

## Yanga' credence paid off, says Kaze



'Medical research will protect health personnel'

PAGE 2



## Focus on service, public leaders told

PAGE 4

Liverp
with F
could
La

# Focus on service, public leaders told

THE government has urged public leaders to focus on solution-oriented approaches in addressing problems rather than specific problems facing the general public.

Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries Development, Prof Elisante Ole Gabriel issued the call here during the 12th symposium of the Hombolo-based Local Government Training Institute (LGTI).

He said leaders don't need to be remembered by their position but rather by their contribution towards addressing challenges that the people face in society.

"If we speak of people's development, we must also highlight the contribution of our leaders," he said. Prof Gabriel was of the view that leaders must lead the people to be active players in social and economic activities in the community.

"It is leaders who can facilitate a smooth transition of economic growth between individuals, communities and the nation," he said.

But he was cautious that the same leaders must strive to adopt a solution-based approach in addressing challenges the community faces.

He suggested some working approaches, which include organizing practical public meetings and dialogue that engage all key players in developing workable solutions.

"This is what people will remember you by. It's not your education status, your position or titles," he emphasized.

LGTI Principal, Dr Mpamilwa Madale explained that the institute resolved to organize the symposium to remind both elected and appointed leaders of their responsibilities in providing services to the public.

He said Tanzania recently conducted its general election, and therefore it is high time the newly elected and appointed public leaders go through a formal training that will help them discharge their duties accordingly.

"Our team of academicians had also conducted various research that will help identify challenges facing the public. This is a good start, because the new leaders will be exposed to people's expectations," he said.

Some areas of focus included health, water, infrastructures and education among others. The training institute vowed to offer a token of between 50,000 and 300,000/- to all researchers for helping unearth undocumented challenges facing the people.

Scanned with CamScanner

# Prof. Gabriel afunda wanachuo Hombolo

Na Augusta Njoji, DODOMA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewafunda wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo jijini Dodoma namna ya kuwa viongozi wanaokidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel alitoa somo hilo alipokuwa akiwasilisha mada iliyohusu nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii anayoiongoza kwenye hafla ya kuwatunuku zawadi wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao na wafanyakazi bora wa chuo hicho.

Alisema katika kipindi ambacho nchi ya Tanzania imeingia katika uchumi wa kati viongozi wanawajibu mkubwa wa kuhakikisha wanakidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel aliongeza kuwa nchi nyingi na taasisi zimekuwa zikikwama kufikia malengo tarajiwa kwa sababu ya kukosa usimamizi mzuri.

"Kuwa na rasilimali ni jambo moja, lakini kusimamia rasilimali hizo ni jambo la muhimu zaidi, taasisi nyingi zimekwama kwa kushindwa kusimamia rasilimali zake ikiwamo rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali miundombinu," alisema Prof. Gabriel.

Aliupongeza uongozi wa Chuo cha Hombolo kwa kusimamia ajenda ya uongozi huku akisema kuwa elimu hiyo wanayoitoa kwa wanafunzi wa chuo hicho itawasaidia wanafunzi hapo mbeleni watakapokuwa viongozi.

Alisema kiongozi yeyote wa kuchaguliwa au kuteuliwa ili awe kiongozi bora, ni muhimu kuzingatia mambo matatu ambayo ni kufahamu hasa anaowaongoza wanamahitaji gani? Pia kiongozi atambue kuwa hatakumbukwa kwa cheo chake bali kwa mchango wake kwa jamii ile anayoiongoza na tatu, awe mtu anayewashirikisha wale anaowaongoza katika kutatua kero zao.

"Washirikishe wale unaowaongoza na ndipo utakapoweza kutatua kero, kiongozi mzuri ni yule anayeona tatizo na kuzibadilisha kuwa fursa, na kwa kufanya hivyo ndipo utaweza kukidhi matarajio ya wale unaowaongoza," alisisitiza Prof. Gabriel.

Scanned with CamScanner